



**SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 2**  
**SOUAHÉLI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 2**  
**SWAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 2**

Friday 23 May 2003 (afternoon)  
Vendredi 23 mai 2003 (après-midi)  
Viernes 23 de mayo de 2003 (tarde)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

---

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. You may include in your answer a discussion of a Part 2 work of the same genre if relevant. Answers which are not based on a discussion of at least two Part 3 works, will not score high marks.

**INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS**

- Ne pas ouvrir cette épreuve avant d'y être autorisé.
- Traiter un seul sujet de composition. Vous devez baser votre réponse sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie que vous avez étudiées. Le cas échéant, vous pouvez inclure dans votre réponse une discussion sur une œuvre du même genre littéraire étudiée dans la 2<sup>e</sup> partie du programme. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie n'obtiendront pas une note élevée.

**INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta deberá basarse en al menos dos de las obras estudiadas en la Parte 3. Se podrán hacer comentarios sobre una obra de la Parte 2 del mismo género, si fuera necesario. Las respuestas que no incluyan una discusión sobre al menos dos obras de la Parte 3 no recibirán notas altas.

*Andika insha juu ya moja ya masuala yafwatayo. Jibu lako lazima liwe juu ya angalau kazi mbili za sehemu ya 3 ulizojitayarisha nazo. Lazima uingize katika jibu lako mjadala wa kazi ya sehemu ya 2 ya utanzu huohuo mmoja kama inavyohusika. Majibu ambayo hayaegemei kwenye mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3 hayatapata alama za juu.*

### **Tamthilia**

#### **1. Ama**

- (a) “Wahusika wakuu katika tamthilia wanasimamia migogoro inayozuka katika tamthilia zenyewe.” Kwa kulinganisha angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii, onyesha vipi wahusika wakuu wanavyoshikamana na migogoro ya kazi hizo.

*Au*

- (b) “Kipengele cha mazungumzo, jinsi yanavyotiririka kumvutia msomaji au hadhira ya watazamaji na jinsi yanavyokwenda vyema na maudhui ya tamthilia yenyewe ni kipengele muhimu sana katika kuamua kufanikiwa au kutofanikiwa kwa kazi yenyewe.” Kwa kutumia kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii, onyesha vipi kipengele cha mazungumzo kinavyoelekea kufanikisha au kutofanikisha kazi zenyewe.

### **Riwaya**

#### **2. Ama**

- (a) Kwa kutumia angalau riwaya mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii, jadili jinsi kipengele cha ‘usimulizi’ kilivyo muhimu katika kuifanya riwaya iwe yenye kuvutia na katika kuchambua na kuendeleza maudhui yanayohusiana na riwaya yenyewe.

*Au*

- (b) “Suala la siasa na mwenendo wa kijamii ni suala muhimu katika fasihi ya Kiafrika.” Kwa kutumia angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii, onyesha jinsi zinavyowiana au kupingana na kauli hii.

### **Ushairi**

#### **3. Ama**

- (a) “Mbinu ya ‘arudhi’: mjumuiiko wa beti na mistari, vipande mistari, mizani na mpangilio wa sauti kama vile vina ni mambo muhimu katika ushairi.” Kwa kiasi gani unaona vipengele hivi vya fani ni muhimu kwa kuibulia fikra na hisia katika mashairi uliyoyasoma.

*Au*

- (b) “Ushairi ni sanaa inayotumia maneno machache kwa kuelezea dhana pana.” Kwa kuchagua baadhi ya mashairi katika angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii, ithibitisha au ikanushe kauli hii na useme kwa nini unakubali au unakataa.

## Riwaya ya Mapenzi

### 4. *Ama*

- (a) “Mapenzi yana pande mbili: tamu na chungu.” Ijadili kauli hii kwa kuitolea mifano katika kazi angalau mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii.

*Au*

- (b) Linganisha kiini cha matatizo ya wahusika wakuu wawili waliyomo katika mapenzi ndani ya kazi angalau mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii na onyesha vipi matatizo haya yamechangia kwako mguso wa riwaya zenyewe kwa ujumla.

## Masuala ya Ujumla

### 5. *Ama*

- (a) Katika angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo, onyesha tofauti juu ya namna waandishi wanavyowasilisha wahusika wa kike na wa kiume.

*Au*

- (b) Katika angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo, onyesha vipi waandishi wake wanavyoonyesha majaribio katika kazi zao na vipi majaribio hayo yanaitikiwa na kwa taathira gani.

*Au*

- (c) Elezea dhana ya ‘mhusika mviringo’ na ‘mhusika bapa’ kwa kutoa mifano kutoka katika angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo.

*Au*

- (d) “Kazi ya fasihi huwa na uhusiano mkubwa na jamii inayohusika.” Ijadili kauli hii kwa kuitolea mifano kutoka katika kazi mbili ulizojitayarisha nazo.